Kurukuu na kuinuka kotoka kwenye rukuu

- Mwenye kuswali atainua mikono yake na alete takbiri hali ya kuinama kwende kwenye rukuu, aiweke mikono yake juu ya magoti yake, huku amekunjua vidole vyake kama kwamba anayashika magoti, asawazishe mgongo wake na kichwa chake katika hali ya kuinama kisha aseme: SUBHANA RABIYAL ADHIIM (Kutakasika ni kwa Mola wangu Aliye Mkubwa)(mara tatu) [Imepokewa na Tirmidhi.].

- Kisha ainuke na aseme (awe ni imamu au mwenye kuswali peke yake): SAMI’A LLAHU LIMAN HAMIDAH (Mwenyezi Mungu Anamsikia yule anayemsifu) [Imepokewa na Tirmidhi.], na hapo wote waseme RABANA WALAKAL HAMDUH (Mola wetu! Sifa njema zote ni zako, kujaa kwa mbingu na kujaa kwa ardhi na kujaa

www.al-feqh.com/sw

vilivyoko baina hizo na kujaa kwa vinginvyo baada ya hizo) [Imepokewa na Tirmidhi.].

Na imependekezwa kuweka mikono juu ya kifua kama alivyofanya katika kusimama kabla .ya kurukuu

www.al-feqh.com/sw